

MTIHANI WA TATHMINI WA KISII YA KATI
KISWAHILI

Karatasi 2

Julai/Agosti 2016

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

1. a) Kuwa kazi yake ni kutumikia jamii yake jikoni **1 x 2 = 2**
 b) Anafanyishwa kazi nyingi ngumu ngumu / amepewa kazi ya jikoni, kulima, kuchanja kuni, kufua na kuteka maji
1 x 2 = 2
 c) Kama aliyepotoka / mwasi / hapendezwi naye / hafurahishwi na anayofanya / ni tisho / mzushi / mshindani n.k.
1 x 2 = 2
 d) i) Nafasi ya mwanamke ni jikoni
 ii) Mwanamke hafai kwenda shuleni
 iii) Mwanamke ana kazi maalum (kupika, kuni, maji n.k.)
 iv) Mwanamke ateswapo hafai kufunua mdomo / afyate ulimi
 v) Hana uwezo wa kujiamulia mambo maishani
 vi) Lazima amzalie bwana watoto
 vii) Lazima mwanamke aolewe **zozote 6 x 1 = 6**
 e) i) Akanyamaza / kimya
 ii) Umaskini / ufakiri / ufukara / uchochole / nyuma kimaendeleo / ulitima
 iii) Kasumba ya kiume / fikra za kiume / kujiona bora kuliko wanawake **3 x 1 = 3**
2. a) i) Alikuwa na mazoea ya kupita pale kila siku
 ii) Alikuwa akimwona mtu aliyekuwa hatingishiki
 iii) Alimwona akiwa amelala vilevile kwa muda mrefu / mwaka nenda mwaka rudi
 iv) Alishangaa kwa mara nyingine tena
 v) Siku moja alikuwa akijipinda kwa mbali akadhani macho yake yanamhadaa
 vi) Alipohakikisha kuwa macho yake yanamdanganya, akaamua kuenda zake
 vii) Alipotazama nyuma alishtuka kumwona mtu yule akigeuka / akafunua macho yake na kuketi / alimwona akiamka
 viii) Alizungumza lugha iliyofanana sana na Kiswahili / aliyoelewa / aliyaelewa aliyokuwa akiyasema **zozote 7 x 1 = 7**
- b) i) Mtu huyo alidai kuwa alikuwa amelala pale tangu jana / kwa siku moja
 ii) Kiumbe yule alivaa ngozi iliyochakaa kwa mpito wa miaka mingi
 iii) Alimkumbusha kuwa alikuwa amelala pale kwa miaka mingi
 iv) Kiumbe yule alimkagua na kusema amevaa kizungu / alikuwa tofauti na vijana aliowazoea
 v) Aligundua kuwa alikuwa amelala kwa karne nzima / moja / miaka mingi **5 x 1 = 5**
3. a) i) Irabu - muundo wa midomo
 - muinuko wa ulimi / mkao
 - sehemu ya ulimi inayohusika
 ii) Konsonanti - hali ya glota
 - ala / mahali pa kutamkia
 - namna / jinsi ya kutamkia **6 x ½ = 3**
- b) M - nafsi tenda
 M - nafsi tendwa
 a - kiishio / kiambishi tamati
 ye - kirejeshi **4 x ½ = 2**
- c) Kwa Magera 2/0
- d) i) ndimi ...
 ii) ndisi ... **2 x 1 = 2**
- e) i) A-WA
 ii) U-YA **2 x 1 = 2**
- f) S - KN + KT
 KN - S
 S - Aliyenituma
 KT - t + N + V + E
 t - ni
 N - mtoto
 V - mchanga
 E - sana **8 x ½ = 4**
- g) Mtoto mweupe amenuna sana **1 x 1 = 1**
- h) Mshale wake ulifungwa kwa unyoya mmoja mweusi 2/0
- i) Sentensi iwe moja na ionyeshe maana hizi
 i) fua - safisha nguo / tengeneza kitu kutokana na madini / ondoa makumbi kwenye nazi
 ii) vua - toa nguo mwilini / samaki majini /

epusha kitu au jambo kutoka kwa matatizo

Mfano: mvuvi alivua samaki kisha akafua nguo zilizochafuka 2/0

- j) i) lizia
ii) nyishia $2 \times 1 = 2$
- j) i) Silabi katika ushairi
ii) Urefu wa kwenda chini
iii) Kwa undani
iv) Kitu kuwa na $zozote 2 \times 1 = 2$
- l) Mwalimu atathmini. Kwa mfano, ungalimchezea (sehemu ya 'ungali' ni lazima itokee katika jibu la mwanafunzi) 2/0
- m) i) kiima - mimi na Juma
ii) muundo - W + U + N $2 \times 1 = 2$
- n) i) Kirai kihusishi
ii) Kirai kielezi $2 \times 1 = 2$
- o) Vile vijoka vilikatwa vikia / vijikia 2/0
- p) Tembo alimfukuza hadi juu ya kichuguu / kidurusi / kingulima / kishirazi $2 \times 1 = 2$
- q) i) Kwa niaba ya (pesa ni za mzazi)
ii) Kwa manufaa ya (pesa ni za mtoto)
iii) Mtoto wake mwenyewe
iv) Mtoto wa mtu mwingine
v) Kuku na kifaranga wake
vi) Yeye na mtoto wake (wote wawili) walinunuliwa kuku $zozote 3 \times 1 = 3$
4. a) i) Ina wazungumzaji wengi
ii) Ni lugha ya mama / kwanza ya kikundi cha watu katika taifa husika
iii) Huwa na muundo wa kiisimu unaofanana na ule wa baadhi ya lugha za watu
iv) Huwa ni lugha mojawapo asilia / si ya kigeni $zozote 3 \times 1 = 3$
- b) i) Huleta umoja wa taifa lote / huunganisha watu
ii) Huwawezesha kufanya kazi kwa pamoja kwa manufaa ya taifa
iii) Ni kifaa cha kuziba mipaka ya kikabila
iv) Hukuza utamaduni wa kiafrika
v) Hukuza uzalendo wa watu wa taifa
vi) Hutambulisha watu wa taifa fulani
vii) Huleta maendeleo ya kijamii / uchumi na kisayansi
viii) Husawazisha watu kilugha kwa kuwa na hisia sawa
ix) Hufanikisha harakati za uongozi $zozote 7 \times 1 = 7$

MTIHANI WA TATHMINI WA KISII YA KATI**KISWAHILI**

Karatasi 3

Julai/Agosti 2016

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA**SEHEMU A : USHAIRI**

1. a) i) Mshairi anadhamiria kuwasuta walimu na wanafunzi dhidi ya wizi wa mtihani
ii) Kukashifu tendo la wizi wa mtihani
- b) i) Vina - ukaraguni - vina vya ukwapi na utao vinabadilikabadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine
ii) Mishororo - tarbia - mishororo minne kila ubeti
- c) Taja madhara ya
i) Kuharibu maisha yako ya kesho - kesho yako motoni
ii) Kufukuzwa / kushindwa kufanya kozi uliyoitwa - kozini ukaungama $2 \times 1 = 2$
- d) Ya nini kuparamia, daraja kuvuka bila $1 \times 2 = 2$
- e) i) Jazanda / sitiari - daraja
ii) Methali - daraja tuvuke kwa karibu tukifika
iii) Msemo - kesho yako motoni
- f) i) Inkisari - kua, ulokutoka wanetu - kuleta urari wa mizani
ii) Mazida - kuharibuni - kuleta urari wa vina
iii) Tabdila - sisumbua - kuleta urari wa vina
iv) Kuboronga / kufinyanga / kubananga sarufi - wa mtihani wizi acha - acha wizi wa mtihani maisha yetu tuguni - tuguni maisha yetu
- kuleta urari wa vina
(mwanafunzi sharti atoe mfano wa uhuru ili apate nusu) nusu nyingine ni ya umuhimu)
- g) i) Kila mshororo umegawika katika vipande viwili, ukwapi na utao
ii) Kila mshororo una mizani kumi na sita
iii) Vina vya ukwapi vinatiririka sawa na vina vya utao (ba, mi, ni, sho)
Tanbihi
i) Sharti mwanafunzi ataje kuwa kinachogawika katika vipande ni kila mshororo
ii) Atakayesema shairi limegawika katika vipande viwili asipate
- h) Ukishapita mtihani ni kozi gani utafanya? Udaktari na uhandisi huwezi kwani ni ndoto isiyowezekana. Baada ya kugunduliwa ulitoroka kozini. Uwazi wako na mimi utaboresha maisha yetu ya kesho $4 \times 1 = 4$
2. a) i) Msemaji - Diwani II
ii) Msemewa - Meya, Diwani I na Bili
(mwanafunzi akisema Meya apate)
iii) Mahali - ofisi mwa Meya
iv) Sababu - wanapanga miradi ya uzalendo
- wanatafuta namna ya kuzima migomo ya wafanyakazi $4 \times 1 = 4$
- b) i) Katili / dhalimu - anapendekeza wafanyakazi kusukumwa kabisa (kutembezewa virungu)
ii) Msaliti - anapendekeza wafanyakazi wasukumwe badala ya vilio vyao kusikizwa
iii) Mshauri mbaya - anamshauri Meya kutumia nguvu kuzima migomo
iv) Kikaragozi - anatoa ushauri wa kumfurahisha Meya bila kuwazia madhara yake (za kwanza $2 \times 2 = 4$)
- c) i) Madiwani wana bima za matibabu katika hospitali kubwa ilhali wanacheneo hawawezi dawa na zikiwepo wanaambiwa kulipia
ii) Watoto wa Meya wanasomea ng'ambo ili wapate elimu ya huko ilhali wanacheneo hawamudu hata karo - wanao wanafukuzwa shuleni
iii) Wanacheneo hawana maji ilhali kwa Meya kuna maji safi
iv) Madiwani wanaongezwa mishahara hata kama zimesalia siku mbili mwezi kukamilika ilhali wafanyakazi wanaambiwa baraza halina pesa
v) Meya anaidhinisha ombi la madiwani kutotozwa kodi ilhali mama muuza ndizi anatozwa kodi
vi) Meya analalamikia viyai vidogo ilhali wanacheneo hawawezi hata kumudu chakula kwani wanapewa chakula kinachopimiwa mbwa na wengine wanakula mizizi na matunda mwiu
vii) Mkewe Meya anapeleka kujifungulia ng'ambo akidai madaktari wa cheneo ni wa kubahatisha ilhali wanacheneo wanakufa kwa kukosa dawa
viii) Madiwani wanataka kuvalia vizuri mbele ya wenzao ilhali wanacheneo hawawezi kumudu gharama ya maisha
ix) Wafanyakazi wanapogoma kushtaki hali zao wanatembezewa virungu **zozote $6 \times 2 = 12$**
3. i) Meya anaendesha baraza kwa kutumia uongo. Anasema kwamba ameagiza dawa ilhali hajaagiza
ii) Anakataa kusikiliza ushauri wa Siki na Diwani III na kuwasikiliza Diwani I, Diwani II na Bili ambao wanampotosha - kuiba fimbo ya Meya
iii) Meya anaidhinisha nyongeza ya mishahara ya madiwani hata kama zimesalia siku mbili mwezi ukamilike
iv) Meya ananyakua viwanja vya ardhi na kumgawia Bili vingine
v) Unafiki wake wa kidini unaligharimu baraza sadaka ya shilingi laki moja kwa mwezi
vi) Uongozi wake unashindwa kuleta uthabiti na usalama wa chakula. Watu wanakufa kwa kula mizizi na matuda mwiu

- vii) Anajilinganisha na majirani dhaifu akisema Cheneo ni kisiwa cha kupigiwa mfano
- viii) Anaupoka uchumi wa nchi kwa kuwapeleka wanawe kusomea ng'ambo akidai elimu ya Cheneo ni ya kawaida mno badala ya kuiboresha kwa kuwa yeye ndiye kiongozi
- ix) Mawazo yake finyu yanamzuia kuona umuhimu wa mpango wa kimaendeleo wa miaka kumi. Yeye anawazia tu malengo ya kimilenia.
- x) Anatomia askari kuwatawanya wafanyakazi wanapogoma kupigania haki zao
- xi) Anashindwa kung'amua udanganyifu wa Bili na kushawishika hata kuiba fimbo ya Meya ambayo ndiyo kitambulisho chake cha Umeya
- xii) Anashindwa kutofautisha baina ya ukasuku / ubarakala wa madiwani wanashirikiananayeili kufaidi mfano wanapomshauri kutembeza virungu wanaomba ovataimu
- xiii) Anatoa maamuzi yanayohusu fedha bila kumhusisha Diwani III ambaye ndiye anayeshughulikia masuala ya fedha
- xiv) Anatomia mbinu hasi za uongozi kama vile propaganda, vitisho na vishawishi mfano nyimbo za kizalendo, mashindano ya vijana n.k.
- xv) Anamwajiri mhazili ambaye hana hitimu zinazofaa
- xvi) Hawazii gharama ya migomo kwa baraza - pato linarudi chini
- xvii) Anamwachilia Bili kumtolea maamuzi muhimu kuhusiana na uongozi wa Baraza
- xviii) Anamtelekeza mji kwenye uchafu kiasi kwamba hata harufu ya uvundo inamzuia yeye mwenyewe kunywa maji
- xix) Maamumi anayotoa yanalenga kutekeleza maslahi yake binafsi. Anawaambia madiwani kwamba hataki kusikia mtu amekufa kwani mizuka yao itamletea tatizo wakati wa uchaguzi
- xx) Analitia baraza kwenye deni na hatia kwa kumpokonya mwanakandarasi kandarasi na kumshauri kulishtaki baraza ili baraza limlipe fidia naye Meya apate mgao wake **zozote 10 x 2**

Tanbihi:

Mwanafunzi aeleze hoja kikamilifu ili apate alama mbili

- lazima ataje mhusika ambaye ni Meya na kitendo chake ambacho kinaonyesha kuwa jina mshtahiki halimfai

4. a) i) Msemaji - Mtemi Nasaba Bora
ii) Msemewa - wanasokomoko
iii) Mahali - uwanja wa Nasaba Bora
iv) Sababu - anawahutubia wanasokomoko katika siku kuu ya wazalendo **4 x 1 = 4**
- b) Kinaya
- Mtemi anasema wanafurahia uhuru ilhali watu hawana uhuru - anamuua mamake Imani na kunyakua shamba lao, anamuua Chichiri Hamadi na kunyakua shamba lake **1 x 2 = 2**
- Tanbihi: Kuhamisha ndimi si tamathali ya usemi
- c) i) Mtemi Nasaba Bora anawatuma askari wake kumpiga na kumwondoa mamake Imani kwenye shamba lao kisha kulichukua
ii) Mtemi Nasaba Bora anawalipa majambazi kumuua Chichiri Hamadi na kulichukua shamba lake
iii) Mtemi Nasaba Bora anamnasabisha Yusufu na kifo cha Chichiri Hamadi na kumsababishia kifungo cha maisha
iv) Mtemi Nasaba Bora anampa Amani kichapo cha mbwa kwa kumtuhumu kumwendea kinyume na Bi Zuhura
v) Mwalimu Majisifu anamwibia Amani mswada na kuuchapisha kwa jina lake
vi) Mtemi Nasaba Bora anampagaza Amani kitoto uhuru
vii) Mtemi anawalazimisha watu kuchanga pesa za kumpeleka madhubuti Urusi kusoma
viii) Wauguzi wa zahanati wanakataa kunitibu kitoto uhuru wakidai ni sikukuu ya uhuru
ix) Mtemi anawafungia Amani na Imani kwa tuhuma za kukiua kitoto uhuru
x) Wazalendo waliopigania nchi wanapuuzwa mfano, Matuko Weye ana Chwechwe Makweche
xi) Mtemi Nasaba Bora anatoa hongo ili mwanaye Madhubuti apate kazi jeshini
xii) Mtemi Nasaba Bora anapofanya kazi katika wizara ya ardhi na makao, anaficha mafaili ili kujipatia milungura
xiii) Mtemi anawalazimisha wanasokomoko kuyachanja majibwa yao lakini yake hayachanjiwi
xiv) Mtemi anakataa kumpeleka DJ hospitalini anapoumwa na mbwa wake Jimmy licha ya kuwa ni sheria
5. i) Benbella anambaka mtoto mdogo
ii) Wauguzi wa hospitali / zahanati ya Nasaba Bora wanakataa kunitibu kitoto uhuru
iii) Imani na Amani wanafungwa kwa tuhuma za kukiua kitoto Uhuru.
iv) Mtemi Nasaba Bora anamkataa mtoto wake Uhuru na kumpagaza Amani
v) Mwalimu Majisifu anawaita wanawe Masimbi na Mashata na hata kutishia kuwarusha majini
vi) Watoto wadogo wanaajiriwa kufanya kazi ya kuchunga mifugo mfano, DJ na wenzake, Imani kuajiriwa kama kijakazi kwa mwalimu Majisifu
vii) Wanafunzi wa shule ya upili ya Nasaba Bora wanakosa kufunzwa somo la Kiswahili muhula mzima na mwalimu Majisifu
viii) Fao anamringa msichana wa shule ya upili ya Kinondani
ix) Fao anaenda ng'ambo kusoma kwa pesa za mahawinde
x) Mtemi Nasaba Bora anampita mama mjamzito aliyekuwa akijifungua - kutomsaidia alikiuka haki za mtoto aliyekuwa akizaliwa
xi) Askari waliotumwa na Mtemi kumpiga mamake Imani wanakiuka haki za Imani na Oscar kambona kwa kumchapa mama yao mbele yao - wanasababisha dhiki yakisaikolojia
xii) Askari wa mtemi wanakiuka haki za Imani na Oscar kambona kwa kuuawa kwa mama yao na hivyo kuwa mayatima
xiii) Mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Nasaba Bora anakiuka haki za wanafunzi kwa kucheza mchezo wa kibe nao
xiv) Mwalimu Majisifu anakiuka haki za wanawe kwa kuwaficha Mashaka anapoingia
xv) Ben Bella anakiuka haki za Mashaka kwa kuhusiana naye akiwa mwanafunzi jambo ambalo linafanya Mashaka kuwehuka

anapoachwa na Ben Bella

xvi) Mtemi Nasaba Bora anakiuka haki za Lowela kwa kufanya mapenzi naye na hali ni mwanafunzi **zozote 10 x 2 = 20**

Tanbihi:

- i) Amani si mtoto, alikuwa na miaka ishirini na minne
- ii) Watoto ni wale waliokuwa chini ya mika kumi na minane

6. a) Mwana wa Darubini : K.M Mbai

- i) Msemaji - Mwatela
- ii) Msemewa - Kananda
- iii) Mahali - katika barua ya kuomba msamaha
- iv) Sababu - ni baada ya Mwakitawa kupotea nyumbani na Mwatela aliuwa na wasiwasi kuwa huenda alijua ukweli au Anajuta aliyomtendea kananda ndio maana anamwandikia barua ya kuomba msamaha **zozote 4 x 1 = 4**
- ii) i) Kananda anakosa karo ya kuendelea na masomo kwa sababu ya uchochole wa wazazi wake na hivyo analazimika kuwa yaya
- ii) Maria anapokea kichap cha mbwa anapodadisi kuhusu ulevi wa Mwatela
- iii) Kananda anatiwa doa na Mwatela wakati Maria alipowatembelea wazazi wake
- iv) Kananda anapokea vitisho vya mauaji kutoka kwa Mwatela iwapo angemwambia Maria kuhusu mimba yake
- v) Kananda anadanganywa na Mwatela kuwa angemuo baada ya kujifungua
- vi) Maria anachomeka vibaya katika harakati zake za kumwoko mwanaye Sami
- vii) Maria anampoteza mwanaye wa kipekee Sami katika mkasa wa moto
- viii) Kananda anapojifungua Mwatela anamnyanganya mwanaye
- ix) Mwatela anapeana Kananda kwa dereva wa malori kutoka Kongo ambaye anaishi naye kama mke kisha kumuua kama mtumwa
- x) Mwatela anamchochea Mwakitawa kumpiga mamake (Kananda) kwa manati **za kwana 6 x 1 = 6**

b) Damu Nyeusi : K. Walibora

- i) Fikirini anaachwa katika kituo cha basi na basi la shule linaloendeshwa na dereva mzungu
- ii) Fikirini anatozwa faini mara mbili na polisi mzungu kwa kuvuka barabara huku taa zikiwa nyekundu ilhali wazungu wanaachiwa wavuke taa zikiwa nyekundu bila kuadhibiwa
- iii) Polisi wanamkamata Fikirini kwa kutofunga zipu na kuishiwa kutozwa faini ya dola mia mbili
- iv) Polisi wanaomkamata Fikirini wanamwona kama mtu asiyejua Kiingereza - wanamuuliza kama alijua kuongea Kiingereza
- v) Fikirini aendapo kununua vitu kwenye maduka makubwa, mlinzi humfuatafuata kana kwamba anamshuku atadoko vitu vya watu
- vi) Wahadhiri wanatoa alama kwa kupendelea watu weupe na kuwakandamiza weusi
- vii) Wanaume weusi hawapati shahada vya vyuoni, wanang'ang'ania kula kalenda
- viii) Fikirini anapoingia mkahawani anakumbana na mitazamo ya dharau ya wateja na wahudumu
- ix) Fikirini anapokuwa darasani mhadhiri mzungu na wanafunzi darasani hawasiti kumsaili maswali ya kumdhaliisha na kumdunisha mfano :
"Je, kule kwenu watu wanavaa nguo au wanatembea rabana?"
- x) Fiona na Bob (wazungu weusi) wanampora Fikirini kila kitu na kutishia kumuua kabla ya kumfukuza akiwa uchi FASIHI SIMULIZI

7. a) Maapizo

- b) i) Hutolewa kwa watu walioenda kinyume na matarajio ya jamii. Mfano: wabakaji, wezi, wauaji n.k.
- ii) Katika baadhi ya jamii maapizo hutolewa kabla ya ulaji viapo
- iii) Maapizo yanaweza kutolewa moja kwa moja na yule aliyethirika mfano; aliyeibiwa
- iv) Katika baadhi ya jamii, watu mahususi waliteuliwa kutoa maapizo hasa wakati wa ulaji kiapo
- v) Kidini, Mungu, miungu au mizimu huweza kutoa maapizo kuhusu mustakabali wa mhusika fulani
- vi) Maapizo huaminiwa kuwa yataleta maangamizi kwa jamii, hivyo wanajamii hushauriwa kuyaepuka kwa kutenda mema
- vii) Maapizo hutumia lugha fasaha (ulumbi). Watoaji maapizo katika ulaji wa viapo aghalabu huwa walumbi
- viii) Maapizo hutumia lugha kali inayonuiwa kujaza woga ili kuonya dhidi ya maovu. Mfano: kama unajua, uliiba mbuzi wangu, mrudishe kabla ya jioni la sivyo utakula nyasi **za kwanza 5 x 2 = 10**

Tanbihi:

- i) Maapizo ni maombi maalum ya kumtaka Mungu / miungu / mizimu kumwadhibu mhusika hasidi, mkinzani au mwovu
- ii) Ni dua ya laana au maombi mabaya kutoka kwa mtu ambaye anahisi ametendewa uovu au amesalitiwa na mwingine
- c) i) Kupitia utohozi mfano; 'windo' - dirisha
- ii) Kufupisha maneno mfano; 'gava' - government
'dere' - dereva
'compe' - competition
- iii) Kutumia sitiari (ufananisho) mfano golikipa kuitwa nyani kutokana na weledi wake; kasuku - anayesema sana au fisi - mlafi
- iv) Kubadilisha maana ya kawaida ya maneno mfano; 'toboa' kwa maana ya kufaulu
- v) Uvumbuzi wa maneno mapya mfano; neno zii! kumaanisha hapana, 'njumu' kwa maana ya viatu
- vi) Kwa kuchanganya lugha mfano; kubeat, kujiwaste
- vii) Kuendeleza maneno kinyume mfano; kumi - 'miku'
enda - 'ndae'

zozote 4 x 2 = 8